S. L. P. 1174
DODOMA, TANZANIA
Barua pepe: info@tastastat.or.tz
Mobile: +255 (0) 754757607
Tovuti: www.tastastat.or.tz

TAARIFA KWA WANACHAMA WOTE KUHUSU MAANDALIZI YA MKUTANO MKUU WA NANE WA CHAMA CHA WATAKWIMU TANZANIA – 2026

Uongozi wa Chama cha Watakwimu Tanzania (TASTA) unapenda kuwataarifu wanachama wote kuwa maandalizi ya Mkutano Mkuu wa Nane wa Chama yanaendelea. Mkutano huo unatarajiwa kufanyika mwezi Novemba 2026 jijini Dodoma.

Aidha, maandalizi yanaendelea ya kuratibu Mkutano Mkuu pamoja na maadhimisho ya Siku ya Takwimu Afrika yanayoandaliwa na Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS), kwa lengo la kuwapa wanachama wa TASTA fursa ya kuhudhuria na kushiriki katika maadhimisho hayo.

Mkutano unatarajiwa kujumuisha shughuli zifuatazo:

1. Uchaguzi wa viongozi wa Chama
   Uchaguzi wa viongozi wa Chama utafanyika kwa kuzingatia masharti ya Ibara ya 43(c) ya Katiba ya TASTA.

2. Mawasilisho ya mada za kitaaluma
Mawasilisho yatakayofanyika yatazingatia mada kuu isemayo: “The Use of Artificial Intelligence (AI) in the Production, Reporting and Dissemination of Statistical Products”.

Wanachama wote wanahimizwa kuanza maandalizi mapema kwa ajili ya kushiriki katika Mkutano Mkuu wa Nane, ikiwemo kujiandaa kwa uchaguzi, kuandaa mada za kitaaluma na kupanga kushiriki katika maadhimisho ya Siku ya Takwimu Afrika.

Taarifa zaidi kuhusu tarehe na utaratibu wa uchaguzi, mwongozo wa uwasilishaji wa mada na mipango ya kushiriki katika maadhimisho ya Siku ya Takwimu Afrika zitatolewa kupitia njia rasmi za mawasiliano za Chama kadiri maandalizi yatakavyoendelea.

Ushiriki wa kila mwanachama ni muhimu katika kufanikisha mkutano huu, kuimarisha umoja wa wanachama na kukuza ushirikiano miongoni mwa wataalamu wa takwimu nchini Tanzania.
Imetolewa na:

UONGOZI WA CHAMA CHA WATAKWIMU TANZANIA (TASTA)
27 OKTOBA 2026